TOLEO NO.73

# Khilafah

SHAWWAL 1447 HIJIRIA —APRILI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## KUMBUKUMBU YA SHIRIKA LA 'WHO' NA HALI YA AFYA TANZANIA




Mwezi huu wa Aprili mwaka 1948 ndio liliundwa Shirika la Afya Duniani (WHO), na ajenda ya afya, changamoto na masuluhisho yake hujadiliwa sana ndani ya mwezi huu katika majukwaa mbali mbali kwa munasaba wa kuundwa Shirika hilo.

Wakati hayo yakijiri kwa upande waTanzania inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalamu wa afya hususan madaktari ambapo uwiano wa madaktari na wagonjwa inakadiriwa kuwa 1:20000. Hali hii ni kinyume na muongozo wa WHO ambapo inataka pawe na uwino wa 1:8000.

Ajabu ni kwamba Tanzania inakadiriwa kuwa na madaktari zaidi ya 22,000. Hata hivyo daktari ambao wapo kwenye ajira ni 8,000-12,000 hivyo kupelekea madaktari wengi kubaki mtaani bila ya kazi.

Hali hiyo pia hupelekea adaktari kufanya kazi zaidi ya masaa 8 kwa siku na kuhudumia zaidi ya wagonjwa 40, kitendo ambacho ni kinyume na muongozo wa WHO ambapo inataka daktar ahudumie wagonjwa 6 kwa siku.

Aidha, hali hiyo hupelekea kuathiriwa kwa dhana ya matibabu kwa sababu daktari anakosa Muda wa kutosha wa kuongea na mgonjwa kama muongozo wa matibabu unavyotaka.

Kwa mujibu wa taaluma ya kitabibu asilimia 85 ya utambuzi wa ugonjwa(diagnosis) hupatikani kupitia mazungumzo (history taking) baina ya daktari na mgonjwa, na asilimia 15 tu ndio hupatikani kupitia vipimo (lab investigation).

Hii ina maana kwa mujibu wa fani ya kitabibu njia ya kuyaelewa magonjwa kwa kutumia akili (rational method) ina nafasi kubwa sana kuliko njia ya kisayansi(scientific method) na

**Inaendelea Uk. 3**

## UBEPARI NDIO CHANZO CHA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI TANZANIA



Mnamo tarehe 4 Machi 2026, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA) ilitoa taarifa kwa Umma jijini Dar es Salaam kwamba imekamata tani 9.93 za aina mbalimbali za dawa za kulevya, chupa 1,795 za dawa za tiba zenye viambata vya dawa za kulevya, pamoja na kuharibu mashamba ya bangi yenye ukubwa wa ekari 87.5 katika operesheni zilizofanyika miezi ya Januari na Februari pekee.

Matumizi ya dawa za kulevya yapo katika maeneo mengi ya Tanzania, hususan katika miji mikubwa. Kwa mujibu wa taasisi ya "Harm Reduction International", takriban watu 30,000 nchini Tanzania hutumia dawa za kulevya kwa kujidunga, kati yao, asilimia 14 wanaishi na virusi vya UKIMWI na asilimia 23.1 wana maambukizi ya Homa ya Ini

**Inaendelea Uk. 5**

## Yaliyomo :


- **Ramadhani imeondoka, majukumu yapo……………………...…..2**
- **Mali iliyoporwa…………………………………...…..……………4**
- **Shawwal na ujasiri wa wanawake……………………………...5**
- **Uqadhi' kwa Upana katika Uislamu……………………………....6**

# TUMEMALIZA RAMADHANI MAJUKUMU YANAENDELEA

Alhamdulillah, tumemaliza mfungo wa Ramadhani na sasa tumo mwezi wa Shawwal.

Licha ya Umma wetu kukabiliwa na kila aina ya mitihani, kuanzia uvamizi kama yanayoendelea Iran, Gaza, Lebanon nk. Pia kukabiliwa na umaskini, mateso kama Kashmiri, Myanmar, Turkistan Mashariki, Sudan nk. Maumivu yote haya yanajiri mbele ya macho ya watawala vibaraka wa nchi za Kiislamu jambo ambalo linatuzidishia machungu kama Umma. Hata hivyo tumeweza kufunga. Allah Taala Atutakabalie swaumu zetu na ibada zote tulizofanya ndani ya mwezi huo. Amiin

Ramadhani imetuachia mazingatio mengi ambayo Waislamu hatuna budi kuyatumia katika masiku haya ya Pasaka, yaani Sikukuu ya Wakiristo.

Hii maana yake Waislamu wajitenge mbali na sherehe hizo za kinasara, wakatae fikra za 'dini mseto' zenye nia ya kuturitadisha kwa kupigia debe kwamba dini zote ni za Mungu. Huu ndio msimamo tuliojengwa na mwezi mtukufu wa Ramadhani wa kusimama juu ya haki na kujiweka mbali na batil,na kutochanganya baina ya haki na batil kwa kuwa Ramadhani ndio mwezi ulioshuka Quran, kitabu cha upambanuzi baina ya haki na batil.

Aidha, Ramadhani inatukumbusha zaidi kuimarisha mahusiano, iwe baina ya Mola wetu au wanadamu wenzetu. Mahusiano baina yetu na Mola wetu ni kwa kufanya ibada mbali mbali



ambazo zimeandaliwa na Allah *Ta'ala* kutuimarishia uhusiano wa moja kwa moja na Yeye. Jambo ambalo ni hitajio letu la kimaumbile la kumnyenyekea Muumba wetu.

Lakini pia tuna mahusiano baina yetu na wanaadamu wenzetu, yaani masuala ya muamalati kama siasa, uchumi, mahusiano baina mwanamume na mwanamke nk. Yote haya yamepangiwa utaratibu maalum na Allah *Ta'ala* kama ilivyo Swaumu ya Ramadhani.

Utaratibu katika mahusiano haya ni lazima kushikamana nao, kama vile tunavyoshikamana na utaratibu katika ibada, kwa kuwa Uislamu haukuyagawa maisha baina ya 'maisha binafsi' (ya kidunia) na 'maisha ya Mungu'. Bali kila kilichoumbwa ni cha Mungu tu bila mshirika, na kwa hivyo mahusiano ya mwanadamu yote lazima yatekelezwe kwa mujibu wa maagizo na utaratibu kutoka Kwake na si vyenginevyo.:

Kwa msingi huo, Uislamu ukatandika nidhamu/ taratibu mbali mbali ili kusimamia na kuongoza mahusiano mema baina ya wanadamu ili kuepuka migongano isiyo ya lazima. Na hili ni kuwa Uislamu sio dini ya *kahanoti* kama vile ukristo au uyahudi yaani dini za kiroho bila nidhamu za maisha.

Uislamu sio tu umeweka nidhamu mbalimbali za kusimamia mahusiano ya binadamu, bali pia ukawajibisha uwepo wa chombo cha kusimamia nidhamu hizo, nacho ni dola ya Khilafah.

Dola ya Khilafah itakuwa na nguvu ya kivitendo kusimamia nidhamu ya mahusiano na Mola wetu, yaani ibada mbali mbali. Bali pia nidhamu za mahusiano ya binadamu iwe katika siasa, uchumi, jamii nk.

Kumalizika Ramadhani sio kumalizika tuliyopata katika Ramadhani. Umma wetu lazima uje na msukumo wa dhati wa kuitikia mwito wa uwajibu wa kurejesha tena dola ya Khilafah ambayo ndio chombo pekee chenye uwezo na mamlaka ya kusimamia vyema mahusiano yote anayohitaji mwanadamu kwa nidhamu thabiti kutoka kwa Muumba wetu.

Allah SWT Anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ .

***"Enyi Mlioamini Muitikieni Allah na Mtume wake anapokuiteni katika jambo la kukupeni uhai" ( Al-Anfal : 24)***

## WHO... *kutoka uk .1*

Kuna umuhimu wa kutanguliza njia ya kiakili kabla ya isayansi.

Lakini Kwa kukosekana wataalamu wa kutosha daktar anakuwa hana muda wa kutosha kufanya mjadala na mgonjwa bali kinachoonekana madaktari wanafanya haraka kuwapeleka wagonjwa kwenye vipimo bila kujua uhalisia wa ugonjwa na vipimo stahiki vya kupima kulingana na tatizo lake.

Madhara ya kutokufuata muongozo huo kunapelekea mgonjwa kupima vipimo ambavyo havihusiani na ugonjwa wake au kufanyiwa vipimo vingi sana bila sababu ya msingi. Jambo linaloongeza uzito wa gharama kwa wagonjwa ambao wengi wao ni masikini. Aidha kufanya vipimo hospitali nyingi bila kutambuliwa ugonjwa. Hivyo, wakati mwengine kupelekea kukosa matibabu stahiki.

Ni fedheha kubwa kwa nchi kama ya Tanzania yenye rasilimali za kutosha kushindwa kuajiri ataalamu wa kutosha wa afya iliyowasomesha kwa gharama. Lakini hilo halishangazi kwa kuwa siasa katika mfumo wa kibepari haipo kuwatumikia watu, bali ipo kutumikia maslahi tu. Ndio maana leo huduma ya afya sio huduma ya kijamii, bali ni biashara kama biashara nyengine.

Dunia inahitaji mfumo mbadala wenye hisia za ubinadamu na unaotumikia raia kikweli, nao sio mwengine bali ni Uislamu tu. Kwa kupitia dola yake ya Khilafah Rashidah utawekeza kwenye kila sekta ya afya kuanzia vituo vya kutosha afya, wataalamu, vifaa tiba,madawa nk. Kwa kuwa jambo hilo ni katika majukumu ya Khalifah katika uchunga na kuwatumikia raia wake, na lau hatofanya ipasavyo atakutana na adhabu kwa Mola wake.

Dr. Masoud Issa

******************

## PASAKA SIO YETU

Uislamu haukatazi kuamiliana na wasiokuwa Waislamu katika masuala ya kiuchumi, kijamii na kibinadamu. Lakini Uislamu haukubali kujumuika au kushirikiana na makafiri katika ibada.

Kwa hivyo, ni haramu Muislamu kusherehekea Pasaka, kwa kuwa ni sherehe yenye mafungamano na imani na ibada ya kikiristo.

Mbali ya kuwa Muislamu ni haramu kusherehekea Pasaka au sherehe nyengine zote za kikafiri, lakini pia kuna madhara mengi:

1.Kunaimarisha fikra hatari ya dini mseto' inayolingania kuzifanya dini zote sawa. Jambao ambalo sio tu linapingwa na dini , bali hata uhalisia.

2.Kuwazoesha (normalize) Waislamu na thaqafa ya kikafiri.

3.Kuondosha msukumo wa Waislamu kuwaona makafiri maadui

4. Kupelekea kuzorota au kuacha kabisa jukumu la Waislamu kuwalingania makafiri. Kwa kuwa watawachukulia dini zote ni sawa.

## MATUKIO YA SHAWWAL

1. Safari ya Mtume kwenda Twaif (Mwaka wa 10 wa Utume)

2. Ambush ya Yemen na Jabbar (Baada ya Vita vya Khaybar)

3. Kufariki dunia mtoto wa Mtume SAAW (Ibrahim bin Rasullulah (29 Shawwal 9 Hijri)

4. Mtume Muhammad SAAW afunga ndoa na Mama Ummu Salamah (ra.) 4 Hijria

5. Vita vya Uhud ( 7 Shawwal Mwaka wa 3 Hijri/ 625)

6. Kuuwawa Shahid Hamza bin 'Abd al-Muttalib 7 Shawal 3 Hijria / 625

7. Kufariki dunia Abu Talib, Ami yake Mtume SAAW katikati ya mwezi wa Shawal 5 kabla ya Hijra.

8. Vita vya Bani Qaynuqaa ( 15 Shawal 2 Hijri/ 624 miladi

9. Vita vya Ahzaab/ Khandaq 17 Shawal Mwaka wa 5 Hijri / 627 miladi )

10. Ambush ya Batn Rabeekh (Mwaka 1.AH kabla ya Vita vya Badr)

11. Vita vya Hunayn ( 10 Shawal Mwaka wa 8.AH)

12. Vita vya Qarqarat al-Kudr 1 Shawal 2 Hijri /623 miladi

13. Vita vya Hamra' al-Asad 8 Shawal 3 Hijria /625

14. Ndoa ya Mtume SAAW na Mama Aisha 1 Shawal 1 Hijria / 623miladi

15. Masahaba wakubwa ya al-Baqi' (Madina) na Jannat ul Mualla (Makka) 8 Shawal 1344/1926

# MALI ILIYOPORWA

**Swali:**

Assalamu Alaykum Warahmatullah Wabarakatuh

Kama inavyojulikana, kuwa ardhi ya Palestina yote imeporwa na kijidola bandia cha mayahudi. Kuna majengo mengi (real estates) na ardhi nyingi zilizoporwa wamiliki hasa hawajulikani. Na baadhi ya ardhi hizi dola ya kiyahudi inawamilikisha watu binafsi au makampuni ili kuwekeza humo miradi yao binafsi, nami naishi Palestina nimeelezwa nikodi real estate (sehemu kwa ajili ya kufanyia biashara ya majengo) katika jengo ambalo analimiliki myahudi kwenye ardhi zilizoporwa katika moja ya vitongoji vya Palestina, na wenye ardhi hii hawajulikani, ima ni wakimbizi au wamehama.

Je inafaa kukodi ***real estate*** hii? Na ikiwa wenye ardhi hasa hawajulikani, je hukmu inabadilika? Au huchukuliwa (inaamiliwa) hiyo kuwa ni ardhi iliyoporwa na haifai kuamiliwa kwa kuiuza, kuinunua au kukodi? Allah Akubariki Sheikh wetu Mkarimu na Akuzidishie nguvu katika kiwiliwili na elimu. Na Allah SWT Afungue kupitia mikono yako.

**Jawabu:**

Waalaykum Salaam Warahmatullah Wabarakatuh,

Ewe ndugu yangu, hakika ya mali iliyoporwa hubakia kuwa ni ya mwenye mali ile, hivyo haifai kuinunua au kuikodi kutoka kwa mporaji. Ufafanuzi wa hayo ni:

Hakika ya mali iliyoibwa au kuporwa huwa ni ya mwenye ile mali popote pale utakapoikuta.



Ametoa Ahmad kutoka kwa Samura amesema: Kasema Mtume (SAAW): ***"Kitakapoibiwa kitu kutoka kwa mtu au kikimpotea mtu kitu chake na akakikuta kwenye mikono ya mtu vilevile kilivyo, basi yeye ndie mwenye haki hasa ya kile kitu. Kisha na arudi mnunuzi kwa muuzaji kwa ajili (ya kuchukua) thamani (yake)".*** *Nass* hii ni kuwa mali iliyoibwa ni haki ya mwenye ile mali. Na pia Mtume (SAAW) anasema: ***"Dhidi ya mkono ulichokichukua mpaka ukirejeshe".*** Ameitoa Tirmidh na akasema hadithi ni *hasan*. Hayo ni kwa mali iliyoporwa.

Kwahiyo, mwenye kupora ardhi ametenda haramu na amechuma dhambi kubwa kwa kauli ya Mtume (SAAW): ***"Mwenye kudhulumu ardhi kiasi cha shibri tu atazongwa kwa ardhi saba".*** Ameitoa Muslim kutoka kwa hadithi ya Aisha (RA). Yaani mwenye kupora sehemu yoyote ya ardhi iwe ndogo au kubwa atakua ametenda dhambi kubwa na ataadhibiwa kwayo Akhera. Na hapa duniani atastahiki adhabu ya *ta'aziir* na atalazimishwa kurejesha alichopora katika hali yake vilevile alivyokipora kwa mwenyewe, kutokana na kauli yake (SAAW): ***"Dhidi ya mkono ulichokichukua mpaka ukirejeshe".*** Ameitoa Tirmidh. Na kikiharibika katika mikono ya mporaji kile kilichoporwa au akakibadilisha hali yake kama kakishona kitambaa kilichoporwa au aliyeyusha madini yaliyoporwa au alichinja mnyama aliyeporwa, basi hudhaminiwa thamani yake na mporaji.

Kwahiyo, ukielewa kwamba kitu kimeibiwa au kimeporwa usikinunue na wala usikikodi na ukiwa (ukihisi) na shubha vilevile usikinunue. Mtume (SAAW) anasema: ***"Wacha lile linalokutia shaka na ulielekee lile lisilokutia shaka".*** Ameitoa Tirmidh kutoka kwa Al Hassan bin Ally (RA). Na Tirmidh akasema "Hadithi hii ni *Hasan na* Sahih.

Kwahiyo, muda wa kwamba una yakini kuwa hiyo ardhi imeporwa, ni sawa ukiwa unamfahamu mwenyewe au humfahamu, la muhimu ni kuwa uwe na uhakika kwamba hiyo imeporwa, itakuwa haifai wewe kuikodi kwasababu mporaji haimiliki, na kwa hivyo hawezi kufunga mkataba ('aqd) wowote na wewe.

Allah SWT akutosheleze na akuepushe na kukodi huko, na tafuta *real estate* nyengine ili ukodi, na Allah akubariki kwayo na itakuwa ni kheri kwako katika dini na dunia. Na kwa vyovyote vile iwavyo hiyo *real estate* usiijutie. Allah yuko pamoja nawe.

Sheikh Ata ibn Khalil Abu Rashta

20, Jamadul akhir 1439H

08/03/2018

aina C (Hepatitis C). Aidha, Tanzania ni njia ya kupitisha dawa za kulevya kimataifa, hasa kupitia bandari na viwanja vya ndege.

Licha ya juhudi za serikali katika kupambana na matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya, kama vile kuanzishwa kwa taasisi za kupambana na dawa za kulevya kama DCEA, kuongezeka kwa vituo vya tiba na urekebishaji wa waathirika kutoka vituo 9 mwaka 2020 hadi 18 mwaka 2025, kuanzishwa kwa programu za matibabu ya kuondoka athari za Uraibu (Methadone), udhibiti wa mipaka, ukamataji wa dawa za kulevya, kampeni za uhamasishaji kwa Umma na hatua nyingine nyingi — bado tatizo hili halijaweza kudhibitiwa. Kwa mfano, mwaka 2020 serikali ilikamata tani 25 za dawa za kulevya, lakini mwaka 2024 zaidi ya tani 2,327 zilikamatwa.

Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine duniani, haiwezi kufanikiwa kupambana na matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya kwa sababu imekumbatia mfumo wa kibepari. Ubepari ambao unayatazama mambo kwa mtazamo wa manufaa binafsi, na hutumia fikra ya Machiavelli ya "matokeo huhalalisha njia", yaani haijalishi kuwadhuru wengine,muhimu tu mtu apate faida na utajiri.

Kutokana na fikra hii ya kishetani ya kibepari, wauza dawa za kulevya duniani kote hupata fedha nyingi sana bila kujali kuwa wanadhuru mamilioni ya watu na kuwaathiri watu wengi ulimwenguni

Kwa upande mwengine, mfumo wa uchumi wa kibepari unasababisha matatizo mengi ya kijamii kiasi kwamba baadhi ya watu hujikuta wakikimbilia dawa za kulevya kama njia ya kujitafutia faraja ya kiuwongo. Bila ya kusahau kuwa waraibu wengine wamehadaiwa na fikra ya ubepari kwamba matumizi ya madawa ya kulevya kuwa ni namna ya kujiletea saada / furaha.

Uislamu umekataza ulevi katika aina zake zote, iwe ni pombe au dawa za kulevya. Uislamu pia umeweka mwongozo wa kimaadili katika jamii unaomfinyanga mtu binafsi na jamii namna ya kushibisha mahitaji yao na kukabiliana na matatizo kama msongo wa mawazo na umaskini bila kuangukia katika mitego ya ulevi na dawa za kulevya.

Kwa kumalizia, mfumo wa kijamii na mfumo wa chumi wa Kiislamu inatoa mwongozo kamili wa namna ya kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, kwa kujenga shakhsia ya Kiislamu na kuweka adhabu kali chini ya Dola ya Khilafah.

**Imeandikwa na Said Bitomwa**
**Mjumbe wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**
**Kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

********************



## MWEZI WA SHAWWAL NA UJASIRI WA WANAWAKE

Mwezi wa Shawwal kuna mengi katika misimamo, muhanga na subra kwa akinamama wa Kiislamu

Shawwal ndio mwezi uliotokea vita kadhaa vikali vilivyowatia Waislamu misukosuko mikubwa na kukabili kwa subra na istiqama na la ajabu zaidi wanawake pia nao walikuwa mstari wa mbele

Vita vya Uhud (Shawwal 3H), wakati wanawake wa kikafiri wakiwatumbuiza kwa nyimbo za mahaba kuwahamasisha makafiri wenzao kuwapiga Waislamu, wanawake wa Kiislamu wao waliwahamasisha waume na kaka zao na Waislamu kwa nasaha kupigana na makafiri na kuridhia qadhaa ya Allah *Ta'ala* kwa yatakayowasibu.

Aidha, baadhi ya wanawake walishiriki kikamilifu kutoa huduma ya mwanzo (first aid) kwa majeruhi. Bi.Fatma (ra) ni mmoja wa mfano bora katika kumuuguza baba yake SAAW majeraha ya vita.

Bibi Safiya bint Abi Talib, shangazi yake Mtume (SAAW) na dada wa bwana wa mashahid Hamza bin Abi Talib RA. aliipokea taarifa ya kuuwawa kaka yake kwa kuridhia qadhaa ya Allah na kwa subra.

Bibi huyu (Bi Safiyya) wakati akiwa na miaka 85 ndiye katika Shawwal 5 H katika Vita vya Ahzaab aliyemuua yahudi muovu, alifanya hayo baada ya Mtume SAAW kutoa agizo kwamba **Uk. 8**

## UQADHI’ KWA UPANA KATIKA UISLAMU

Baada ya makafiri kushtushwa na kustaajabishwa na ujasiri wa hali ya juu na ushindi mkubwa wa Waislamu wa kupambana kwa kufungua (Fat-hi) kwao miji hususan katika karne ya 7 Hijria (karne ya 13 miladi) walianza kutanabahi kwamba vita vya medani ya kisilaha pekee havitotesheleza kuwamaliza Waislamu, bali lazima wahijuhisishe pia katika uwanja wa vita vya kifikra. Vita ambavyo ni vya hatari zaidi na vilivyoacha na kuendeleza athari kubwa.

Vita hivi vililenga kuigonga moja kwa moja aqeeda ya Kiislamu na kutengeneza ufahamu wa kimakosa katika fikra mbali mbali za Kiislamu ili kuondoa nishati na kufuta msimamo na thiqa [confidence] ya Waislamu juu ya dini yao.

Miongoni mwa fikra walizozivamia makafiri kikatili na kuzipotoa kwa makusudi ili kuwachanganya Waislamu ni fikra ya Jihadi, Dola ya Khilafah na ‘Sheria ya Kiislamu’ ndani yake ikihusisha suala zima la ‘Uqadhi’ ambalo mabakibaki yake bado hupatikana katika baadhi ya maeneo ya Waislamu katika biladi kadhaa ndani ya Bara Arabu, Bara Hindi, Afrika Mashariki, ikiwemo Kenya, Zanzibar nk.

Tamko la ‘Uqadhi’ kilugha linatokana na neno ‘Qadha’ ambalo limetumika mara nyingi ndani ya Qurani Tukufu miongoni mwa maana zake ni kama hizi.

Kukata shauri kama katika aya:

قُضِيَ الْأَمْرُ الَّذِي فِيهِ تَسْتَفْتِيَانِ

“Limeshakatwa shauri jambo mlilokuwa mkiuliza..”



[TMQ Yusuf:41]

2. Kuhukumu

وَاللَّهُ يَقْضِي بِالْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَقْضُونَ بِشَيْءٍ إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِير

Na Allah huhukumu kwa haki lakini wale mnaowaabudu kinyume na Allah hawahukumu chochote” [TMQ 40:20]

3. Kutoa agizo

وَقَضَى رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola wako ameagiza msimwabudu yoyote ila Yeye tu, na pia kuwafanyia wema wazee wawili” [TMQ 17:23]

4. Kukamilisha jambo,muda, kitu kama kulipa deni nk.kama katika aya zifuatazo:

فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَاسِكَكُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا

‘Na mnapomaliza ibada zenu za hijja basi mtajeni Allah kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu bali mtajeni zaidi’ [TMQ 2:200]

Pia kwa maana kama hiyo hupatikana katika aya

فَلَمَّا قَضَى مُوسَى الْأَجَلَ وَسَارَ بِأَهْلِهِ

“’Basi Mussa alipotimiza muda alisafiri pamoja na ahli zake’…

[TMQ 28:29]

Amma ki-Sheria/kiistlahi, tamko la ’Uqadhi’ ni utoaji wa hukmu kwa njia ya kulazimisha. Kwanza, hukmu inayopambanua mivutano baina ya watu wa kawaida katika masuala jumla [Amm] ya Muamalat kama vile ndoa, mirathi, mikataba ya kazi nk . Pili, utoaji wa hukmu yenye kuzuiya kudhuriwa kwa haki ya jamii kwa ujumla wake [Hisba] kama kuzuia kughushi, kusimamia vipimo, kuzuia maeneo ya umma [public places] kutumiwa na wachache nk. Na tatu, ni utowaji wa hukmu ya kuondoa mzozo baina ya raia wa kawaida na yoyote katika ngazi ya utawala [Madhalim] akiwa Khalifah, Msaidizi wake, Wali, Amil au mtumishi yoyote wa serikali.

[‘Nguzo zaDola ya Khilafah’ uk.64].

Alilitumia Mtume [SAAW] tamko hili kuashiria maana ya ‘Utowaji wa hukmu kwa njia ya kulazimisha’ pale alipomteuwa Ali [ra] kumpa jukumu la uqadhi ndani ya Yemen aliposema [SAAW] kumueleza:

»إِذَا تقَاضَى إِلَيْكَ رَجُلَانِ، فَلَا تَقْضِ لِلْأَوَّلِ حَتى تَسمَعَ كَلَامَ الآخَرِ فَسَوْفَ تَدْرِي كَيْفَ تَقْضِي«

“Wakikujia watu wawili ili uwahukumu basi usimhukumu wa mwanzo mpaka umsikilize wa pili, ndipo utakapojua vipi utatoa hukmu.” [Tirmidhi na Ahmad]

Kwa hivyo, kwa mujibu wa maana ya Uqadhi ki-Sheria, katika Uislamu hupatikana maqadhi wa aina tatu:

A.Qadhi Amm [jumla jamala] wa Muamalat/mahusiano ya watu na Uqubat [adhabu za wahalifu] ambae hukaa mahkamani kutatua mizozo

**Inaendelea uk...7**

katika masuala na husuma mbali zinazohusu maisha ya kila siku ya watu kama ndoa, urithi, mikataba baina yao, talaka, matunzo ya watoto nk.

B. Qadhi Muhtasib yeye na jopo la wasaidizi wake husimamia kusipatikanwe kudhuriwa haki ya jamii na maslahi ya jamii kwa ujumla kwa kuangalia na kukagua mambo kama vipimo, maeneo ya umma yasimilikiwe na watu binafsi nk. Qadhi huyu na wasaidizi wake hutoa hukumu papo hapo ya kuzuia kudhuru na haketi mahkamani kusubiri mashtaka bali huyatafuta yanayodhuru umma na kuyachukulia hatua kwa kuyazuia.

C. Na Qadhi Madhalim ambae hujihusisha moja kwa moja kuzuia dhulma ya watawala kwa raia. Qadhi huyu ni wa daraja ya juu kiasi kwamba anaweza kumuuzulu Khalifah katika madaraka ikiwa amekiuka mipaka ya Kiislamu na ndio maana Qadhi huyu licha ya kuwa awe na sifa ya kuwa Muislamu, Balegh, Aqil [mwenye akili], Faqih [mjuzi wa Sheria za Kiislamu], awe huru na Muadilifu ambazo ndizo sifa za maqadhi wote isipokuwa qadhi mkuu ambae hupaswa awe mwanamme pia na yeye qadhi madhalim hulazimika awe Mwanamme na Mujtahid asie khofu lawama ya mwenye kulaumu.

'Uqadhi' katika Uislamu ni mmoja kati ya mihimili kumi na tatu ya Dola [ Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah uk.6 ] na ni wajibu kuwepo kwake kwa sababu ni wajibu kuhukumiwa kwa yale yote aliyoyateremsha Allah Ta'ala kwa dalili nyingi ndani ya Qur'ani na Sunna (kauli na vitendo vya Mtume [SAAW]). Allah Ta'ala anasema:

وَأَنْ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ

Na hukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allah

وإذَا دُعوا إلى اللهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ

"Na wakiitwa kwa Allah na Mtume wake ili wawahukumu baina yao" (TMQ: 24:48)

Amma kwa upande mwengine, pia Mtume [SAAW] mwenyewe alikuwa Qadhi akihukumu watu katika mizozo mbalimbali na akiteuwa maqadhi kama alivyomteua Saydna Ali [ra] awe qadhi wa Yemen, Muadh bin Jabal kuwa qadhi wa Al-Janad pia Saad bin Al-Ass kuwa qadhi wa Hisbah katika soko la Makka baada ya kuifungua [fathi] nk. Na Makhalifa baada yake waliandama mwendo huo huo kuwa maqadhi na kuteuwa maqadhi kwa maeneo mbalimbali kama Umar [ra] alivyomteuwa Abdullah bin Utbah kuwa Qadhi wa hisba soko la Madina.

Maqadhi huchaguliwa moja kwa moja na Khalifah na kulipwa mishahara yao na Dola kama ilivyothibiti kutoka kwa Mtume (SAAW) na Makhalifa. Pia anaweza kupewa mamlaka Qadhi mkuu kuteuwa maqadhi wengine kwa amri ya Khalifah, na endapo jukumu la kuteuwa Qadhi Madhalim pia atapewa Qadhi mkuu kwa niaba ya Khalifah, hulazimika pia nae Qadhi Mkuu kuwa na sifa ya nyongeza ya kuwa Mujtahid.

Pamoja na kwamba Khalifah ana mamlaka ya moja kawa moja ya kuweka na kuondoa maqadhi, mamlaka ya kumuondosha Qadhi Madhalim hubatilika wakati anapokuwa Qadhi huyo yumo katika kesi ya kumchunguza Khalifah au yoyote katika ngazi ya utawala. Katika hali hiyo hawezi kumuachisha kazi.

Hakuna Qadhi wa rufaa katika Uislamu kwani hukmu ya Qadhi huchukuliwa kuwa ndio hukmu ya Mwenyezi Mungu katika qadhia husika na kwa hivyo hakuna anayeweza kuketi katika rufaa kupinga hukmu ya Mwenyezi Mungu. Kilichopo ni uwezekano wa kuketi maqadhi wawili au zaidi pamoja katika kuliangalia kwa kutoa rai juu ya shauri fulani na kukusanya ushahidi, lakini mamlaka ya kukata hukmu huwa kwa Qadhi mmoja tu, waliosalia huwa washauri , na anapokata hukmu huwa hiyo ndiyo hukmu inayowafunga wote [binding] na wala haikatiwi rufaa.

VIPI UQADHI WETU WA LEO ?

Kwa bahati mbaya leo Uqadhi tulionao lazima tukiri na tukubali kwa udhati kabisa, kwamba siyo Uqadhi kwa uhalisia na upana wake kama inavyotaka Sheria ya Kiislamu, pamoja na kwamba Waislamu huruhusiwa kuutumia na kufaidika kwa huu unaoitwa uqadhi katika kupata ushauri na usuluhishi wa husuma zao katika nchi ya Darul kufr [nchi isiyotawaliwa Kiislamu] kama tulivyo leo. Mfano biladi za kiarabu, Pakistan, Zanzibar, Kenya nk.

Hata hivyo lazima iwe bayana kuwa msingi unaosimamia mahkama hizi zinazoitwa za qadhi leo ni msingi dhaifu, legelege na batil unaotokana na

**Inaendelea uk 8**

Uqadhi..kutoka uk 7

msingi wa sheria ya kiingereza unaozichukulia Mila na Desturi za watu kwamba zinaweza kuingizwa [accommodated] ndani ya sheria kuu na kufanywa sheria za kimila [customary law] kwa sharti kwamba kwa mtazamo wao zisiwe za kishenzi [repugnant] na haziathiri kupingana na sheria nyingine. Kwa maneno mengine ya mkato, sheria hizo zikubaliane moja kwa moja na zisiathiri Katiba ya kiilmania [secular constitution].

Msingi huu ndio waliosimamia Waingereza wakati wote, kwa sababu mfumo wao wa kibepari [Urasilmali] umejengwa juu ya msingi huo wa ilmania [secularism] na ndio msingi huo uliomsukuma Gavana wa Uingereza ndani ya Tanganyika katika mwaka 1920 kuagiza iasisiwe Mahkama ya Qadhi ndani ya Tanganyika. Na halkadhalika kwa sababu nchi zetu baada ya uhuru (wa bandia) zinaendelea kujifunga na/kushikilia [adopt] mfumo wa sheria za kiengereza, hapana shaka yoyote kwamba ndio msingi huo pia ndio uliomfanya Raisi Kenyatta kufikia muwafaka na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Zanzibar Mohammed Shamte katika Mwaka 1963 wa kuiwachia Mahkama ya Qadhi iendelee kuwepo ndani ya Kenya na hatimae kuingizwa rasmi ndani ya kifungu cha 66 cha Katiba ya Kenya. Pia ndio msingi huo huo ndio unaofanya pia kuendelea kuwepo kwa Mahkama ya Qadhi ndani ya Zanzibar kwa kumakinishwa chini ya sheria ya Ukadhi ya Mwaka 1985 [The Kadhi's Court Act 1985] na daima ndio msingi huo huo tena utakaotumika kuasisi Mahkama kama hiyo mahala pengine popote chini ya mfumo wa serikali za kiilmania [secular government].

Na zaidi msingi huo huo ndio uliozifanya Mahkama hizi kuwa aibu na fedheha isiyoelezeka kiasi kwamba Mahkama ya Qadhi ya Zanzibar na ile ya Kenya katika kesi za rufaa hulazimu Kadhi Mkuu na baadhi ya Masheikh kuketi meza moja na Majaji wa Mahkama kuu za kiilmania [secular] ati kutoa uamuzi kwa hukumu za Kiislamu, huku inaeleweka wazi na bayana kabisa kwamba sifa ya kuwa Jaji katika Mahkama kuu si Uislamu wala ujuzi wa Sheria za Kiislamu [faqih] bali ni uzoefu wa muda mrefu na kuwa na shahada ya juu ya sheria za kiilmania [LLB].

Umma wetu mtukufu wa Kiislamu hapa Afrika ya Mashariki na dunia nzima una kila sababu kwa hoja za kidini na ki-hali halisi [reality] kutojivunia kamwe na kutoridhika kabisa na aina hii ya Uqadhi unaoruhusiwa na nidhamu ya kiilmania. Kadhalika una kila sababu ya kufanya kazi na kusimama kidete katika kurejesha Khilafah si tu kuja kusimamia Uqadhi pekee kwa upana, haki na uadilifu, bali kuja kuwaokoa na kuwakomboa Waislamu na wasiokuwa Waislamu kutokana na kila aina ya uduni na idhilali na kuwainua katika upeo wa mafanikio na utukufu.




Ujasiri… Kutoka uk. 5

katika vita vile kwamba wanawake wote wakusanywe katika ngome maalum chini ya ulinzi wa sahaba Hassan bin Thabit. Yahudi huyu alikuja kinyemela kufanya ujasusi.

Aidha,bi Himnah bint Jahsh (Ra.) baada ya kupata taarifa ya kuuwawa kaka yake Abdallah bin Jahsh, na pia kuwawa mumewe Musab bin Umair katika Vita vya Uhud aliipokea misiba hiyo kwa subra ya hali ya juu.

Kadhalika, mwanamke mmoja wa kabila la Bani Dinar alipopewa taarifa juu ya kufa shahid katika vita vya Uhud kaka yake na mumewe, aliuliza: *Vipi hali ya Mtume SAAW yukoje*? akajibiwa yuko hai na salama, mama huyo akaomba amuone Mtume SAAW kwa macho yake, na akaoneshwa. Hapo akajibu: '*Msiba wote huu si chochote kwangu kwa kuwa wewe (Mtume SAAW) uko salama'*.

Bila ya kumsahau Ummu Saad (Ra) alipopewa taarifa na Mtume SAAW juu ya kufa shahid mumewe Amr ibn Muadh nae alijibu kama Himnah bint Jahsh. Mtume SAAW akawaombea dua wote waliondokewa na jamaa zao,kisha akamueleza Ummu Saad: '*Furahi ewe* Ummu Saad na wape *bishara wote ambao jamaa zao wamekufa katika Uhud, hao (mashahid) watakuwa nami katika Jannah'*. Ummu Saad akajibu: *''Tumeridhika ewe Mjumbe wa Allah, nani tena atakaewalilia baada ya habari hizi njema'*.

Akinamama wa Kiislamu leo ni wajibu kujipamba na sifa na mwenendo kama huu wa waliotangulia ambao Allah *Ta'ala* aliwaridhia katika dunia hii, na akhera watakuwa kwenye makaazi ya Jannah.